**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UCHUKUZI**

**MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI**

LATRA

IMETHIBITISHWA ISO 9001

# TAARIFA KWA UMMA

## FURSA ZA LESENI ZA MUDA MFUPI KIPINDI CHA MWISHO WA MWAKA

***Dar es Salaam, 03 Desemba, 2025***

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inatangaza fursa kwa wamiliki wa mabasi kuwasilisha maombi ya leseni za muda mfupi ili kuongeza huduma za usafiri wa abiria kwenye njia zenye uhitaji mkubwa kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka.

Leseni hizo zinatolewa kuanzia tarehe 03 Desemba, 2025 kwa kuzingatia;

i) Basi liwe na uwezo wa kubeba abiria kuanzia arobaini (40) au liwe na leseni ya Mabasi Maalum ya Kukodi (Special Hire),
ii) Basi liunganishwe kwenye Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS),
iii) Basi liwe na Bima iliyo hai,
iv) Basi liwe na Hati ya Ukaguzi kutoka Jeshi la Polisi (VIR),
v) Basi liwe na leseni hai ya LATRA,
vi) Dereva awe amesajiliwa na kuthibitishwa na LATRA,
vii) Dereva awe na Kitufe cha Utambuzi (i-button) kilichosajiliwa na LATRA,
viii) Basi liunganishwe kwenye Mfumo wa Safari Tiketi (Tiketi Mtandao).

Maombi yote yatumwe kupitia Mfumo wa Leseni (***rrims.latra.go.tz)*** na nyaraka zifuatazo ziambatishwe;

i) Nakala ya Kadi ya gari,
ii) Nakala ya Hati ya Bima,
iii) Nakala ya Ukaguzi wa gari kutoka Jeshi la Polisi,
iv) Nakala ya Leseni ya Udereva.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi bila malipo kupitia simu namba **0800110019** au **0800110020** au fika ofisi za LATRA zilizopo Stendi Kuu ya Mabasi ya Magufuli na mikoa yote Tanzania Bara.

Digitally Signed By Salum PAZZY
Thu Dec 04 08:27:55 EAT 2025

Salum PAZZY

**MKUU WA KITENGO CHA UHUSIANO NA MAWASILIANO**